

## Maudhi madogo madogo

Baadhi ya maudhi madogo madogo ya chanjo hii ni:

- Maumivu kidogo sehemu chanjo ilipochoywa .
- Kupata wekundu sehemu chanjo ilipotolewa
- Homa baada ya kuchanjwa, kama inavyotokea kwenye chanjo nyingine

Msaada na usahuri waweza kutolewa na watoa huduma za afya pale inapotakiwa.

*Kama una maswali yoyote au dukuduku tafadhali muone mtoa huduma ya afya*

## Chanjo ni Haki ya Kila Msichana wa darasa la nne na wasiokuwa shuleni wenye umri wa miaka 9

Hakikisha binti yako anapata chanjo.

Kwa maelezo zaidi au maswali yoyote tafadhali wasiliana.

Mpango wa Taifa wa Chanjo  
Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii  
Simu: 255 22 2450089  
Fax: 255 2450089



## Jikinge na Saratani ya mlango wa Kizazi




**Mpeleke binti yako akapate Chanjo!**



## Saratani ya mlango wa kizazi – mambo muhimu.

- Mlango wa kizazi ( cervix) ni kiungo katika tumbo la uzazi la mwanamke (angalia picha hapo chini).



- Saratani ya mlango wa kizazi inasababishwa na virusi vijulikanavyo kitaalam kama human papillomavirus (HPV).
- Saratani ya mlango wa kizazi ni ugonjwa hatari na unaua wanawake wengi nchini zinazoendelea.
- HPV huambukizwa kwa njia ya Ngoni toka kwa mtu mwenye virusi hivyo. Virusi hivi pia huambukiza koo au puru kwa jamii zinazofanya ngono za mdomoni na puru
- Maambukizi ya HPV yameenea sana ulimwenguni. KILA MTU akianza kushiriki ngono anakuwa katika hatari ya maambukizi ya virusi vya HPV.
- Tafiti zinaonyesha kuwa, katika kila wanawake wanne wanaoshiriki ngono watatu wanapata maambukizi ya HPV wakati fulani wa maisha yao.
- Wasichana wenye umri mdogo wanao uwezekano mkubwa wa kupata maambukizi ya HPV.

## Dalili za Maambukizi ya HPV

- Baadhi ya dalili za awali za maambukizi ya HPV ni vivimbe kwenye sehemu za uke au Uume; (au koo / puru) vijulikanavyo kama viotea.
- Dalili za Baadae ni mabadiliko katika seli za mlango wa kizazi, ambazo ni dalili za awali za saratani ya mlango wa kizazi
- Mabadiliko haya yasipodhibitiwa mapema hugeuka kuwa saratani ya mlango wa kizazi au viungo vingine

## Dalili za Saratani ya Mlango wa Kizazi

Awali Saratani ya mlango wa kizazi ni haina dalili. Hugundulika tu kwa kuchunguzwa na wataalam wa aafya. Dalili za baadae ni:

- Kutokwa na uchafu na / au damu kwenye uke
- Kupata hedhi bila mpangilio maalumu
- Kutokwa na damu ukeni baada ya tendo la ngono

## Chanjo ya Kukinga Saratani ya Mlango wa Kizazi (HPV)

- Chanjo ya HPV inakinga maambukizi ya virusi vya HPV vinavyosababisha saratani ya mlango wa kizazi
- Chanjo ya HPV inatolewa mara mbili ili kupata kinga kamili
- Chanjo hii inaweza kupunguza matukio ya Saratani ya mlango wa kizazi kwa asilimia 70.
- Chanjo hii ni salama, imethibitishwa na Wizara ya Afya na ustawi wa jamii na Shirika la Afya Duniani.

## Chanjo itatolewaje?

- Chanjo itatolewa na watumishi wa afya kwa kushirikiana na walimu katika shule za Msingi na vituo vya kutolea huduma za afya kwa walengwa wasiokuwa shuleni



- Chanjo itatolewa kwa wasichana wa darasa la nne wenye miaka 9 au zaidi na
- Kwa wasiokuwa shuleni, chanjo itatolewa kwa wasichana wenye umri wa miaka 9 tu.
- Ili kukamilisha kinga, walengwa watahitaji kupata dozi 2 za chanjo hii katika kipindi cha miezi 6

Kumbuka ni muhimu kukamilisha dozi zote

- Chanjo hii inatolewa bila malipo
- Chanjo hii ni salama.